Title 1 ni Nini?

- Ni ruzuku (au msaada wa kifedha) kutoka serkali kuu ya taifa.
- Ni ruzuku (au msaada wa kifedha) toka serkali kuu ya taifa ambayo Shule za Umma za Kaunti ya Fayette zinapokea.

Title 1 inafanya kazi vipi?

- Serikali kuu hutoa ufadhili ku shule za Wilaya kila mwaka.
- Wilaya za shule zinatambua shule ambazo zinastahiki kupokea fedha.

Shule za Title 1 zafanya kazi kwa:

- kutambua wanafunzi wanaohitaji msaada wa kielimu zaidi
- kuweka malengo ya kuboresha
- kupima maendeleo ya mwanafunzi, kulingana na KAS/CCR
- kutengeneza programu zinazoongeza mafundisho ya kawaida darasani
- kushirikisha wazazi katika nyanja zote za programu

Aina mbili za mipango ya Title 1

- **Schoolwide programs**
  Mipango ya shule zote: shule zilizo na 40% au zaidi ya watoto waanotoka ndani ya familia zenye pato ya chini zinaweza kukuza mipango ya Title 1 kwa kuhudumia wanafunzi wote. Mipango ya shule zote zinaweza kuchanganya fedha za Title 1 na fedha za serkali kuu, serikali ya Wilaya, na za mitaa kwa kuboresha programu za shule.
- **Programu zinazolengwa za usaidizi**
  Shule zilizo na 35-39% ya watoto wa kutoka kwa familia zenye kipato cha chini zinaweza kuwa na Mpango wa Usaidizi Unaolengwa. Shule hizi zitahakikisha kuwa watoto wanaohudumiwa na Title 1 waeneze viwango vya ufaulu vya KY. Mipango ya msaada iliyolengwa haiwezi kuchanganya fedha za serkali kuu, serikali ya jimbo, na fedha za mitaa.

Kama mzazi, wewe ni sehemu ya Timu ya Title 1!

- **Muungano wa shule na wazazi** inahamuru malengo na majukumu ya wazazi na shule.
- **Sera ya ushirika wa mzazi na familia** inasaidia wazazi kuelewa na kushiriki katika juhudi za shule.

Ruzuku ya Title 1 ya Shule Letu

- Ruzuku ya Title 1 ya Shule letu kwa mwaka 2020- 2021 ni $ 399, 000 ambazo zinalipa walimu 5. Inalipa pia maendeleo ya kitaalam, vifaa vya kufundishia na vifaa zaidi vya kufundishia.
- Shule yetu ina Programu ya Title 1 ya Shule mzima ambayo inazingatia kuboresha mafanikio ya mwanafunzi katika maeneo yote ya masomo.

Kocha wa Mitaala

- Anasaidia waalimu kwa kuonyesha upangaji na ufundishaji wa masomo.
- Anafundisha kusoma na / au hesabu kwa wanafunzi katika vikundi vidogo.

Waalimu wa Hafla

- Wanafunzi wanapokea huduma ndogo ya kikundi kidogo cha watu 2 na / au watu 3 katika elimu za kusoma na/au za hesabu.

Walimu wa Kurekebisha Usomi / wa Usomi na Uandishi

- Wanafunzi wa darasa la kwanza hupokea somo la nusu saa kila siku kutoka kwa Mwalimu wa Kurekebisha Usomi kwa mda wa wiki 12 hadi 20.
- Wanafunzi wa ELL na wa Mafundisho Maalum hupokea somo la nusu saa kila siku kutoka kwa Mwalimu wa Usomi na Uandishi hadi mpango uishe na ulete mafanikiyo.

Shule yetu inakuhitaji!

- Jifunze kuhusu mpango wako wa Title 1.
- Hudhuria hafla za shule.
- Tembelea madarasa.
- Jitolee kwa kusaidia.
- Jiunge na mashirika ya wazazi.
- Hudhuria mikutano ya mzazi na mwalimu.
- Endelea kuwajulisha waalimu juu ya hafla ambazo zinaweza kuathiri kazi au tabia ya mtoto wako.